

## IDARA YA USIMAMIZI NA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI YA KILIMO

Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo inatoa huduma mbalimbali kama zifuatavyo:-

### 1. Taarifa za maeneo ya uwekezaji wa kilimo:

Idara ya Usimamizi na Mipango ya Ardhi ya Kilimo inajukumu la kutambua na kupima maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo nchini. Utambuzi huu unahusisha kupata taarifa mbalimbali za maeneo yanayofaa kwa kilimo na kuhifadhi taarifa hizo kwenye kanzidata kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Taarifa hizo zinasaidia katika kupendekeza maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kilimo na program mbalimbali zinazochochea uendelezaji wa shughuli za kilimo nchini, mfano Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT).

Hadi kufika Juni, 2023, Idara imeainisha, kutenga, kupima na kuweka mawe ya upimaji kwa ajili hatimiliki katika mashamba makubwa ya pamoja 26 yenye jumla ya ekari 264,841.5 katika Mikoa ya Kigoma (ekari 36,719.75), Mbeya (ekari 52,165), Njombe (ekari 87,000), , Dodoma (ekari 33,453) na Kagera (ekari 5,503.75) Aidha, Wizara inaendelea kuainisha mashamba makubwa ya pamoja na kuhamasisha Sekta binafsi kuanzisha na kuwekeza katika mashamba makubwa ya pamoja.

Vilevile, Wizara kupitia Idara ya Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya ardhi ya kilimo, imetambua maeneo ya kilimo katika mikoa 9 (Kigoma, Singida, Rukwa, Tabora, Lindi, Mtwara, Pwani, Manyarana Ruvuma) yenye zaidi ya hekta 178,000 kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo. Kadhalika, Wizara imepima afya ya udongo katika mashamba hayo ilikushauri mazao yanayostahiki na matumizi sahihi yambolea.

### 2. Miongozo ya Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo:

Miongoni mwa majukumu ya Idara ni pamoja na kuandaa Miongozo mbalimbali inayohusu utunzaji na usimamizi wa ardhi ya kilimo nchini. Kwa sasa Idara ya Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo kwa kushirikiana na SAGCOT inaendelea na kazi ya kuboresha rasimu ya Mwongozo wa namna bora ya kutibu udongo ulioathirika na tindikali, ambapo Mwongozo huo utasaidia Maofisa ugani na wakulima kurejesha rutu baya udongo ulioathirika na tindikali. Aidha, Rasimu ya Mwongozo huo inatarajiwa kuwasilishwa kwenye Menejimenti ya Wizara mwezi Julai kwa ajili ya maboresho na kuanza kutumika.

### 3. Ushauri na Mafunzo ya Kitaalam ya Ardhi ya Kilimo:

Idara inatoa mafunzo kuhusu utunzaji wa ardhi ya kilimo kwa maafisa ugani na wadau mbalimbali wa kilimo nchini. Mafunzo hayo ni pamoja na teknolojia za kuhifadhi maji na udongo mashambani na kuzuia mmomonyoko wa udongo kwenye maeneo ya kilimo. Mafunzo mbalimbali yamefanyi kakatika mikoa ya nyanda za juukusini (Mbeya na Songwe) na kaskazini (Kilimanjaro, Manyarana Tanga)na pia kuwapati aujuzi wa namna bora ya kutibu udongo ulioathrika na tindikali.